# Taarifa ya Sera ya Desturi za Ushirikishaji wa Wazazi

**Iowa City Community School District**
1725 North Dodge Street • Iowa City, IA 52245 • (319) 688-1000 • Faksi (319) 688-1009
www.iowacityschools.org

Ni sera ya Iowa City Community Schools kwamba wazazi na wanafamilia wa watoto wanaoshiriki kupata nafasi ya kushirikishwa pamoja katika maendeleo ya mpango wa wilaya na katika mchakato wa mapitio ya wilaya kwa madhumuni ya uboreshaji wa shule. Kutambua kuwa ushirkishaji wa wazazi ni muhimu kwa ufanisi wa elimu, tunapanga kuwashirikisha wazazi katika ushirikiano wa kufana wa nyumbani na shuleni utakaotoa elimu bora inayowezekana kwa wanafunzi wetu. Wilaya inaratibu, kutoa usaidizi wa kiufundi na misaada mingine muhimu ili kusaidia kwa mipango na utekelezaji wa shughuli za ushirikishaji wa wazazi. Wilaya inahimiza ushirikishaji wa wazazi na kuunga mkono ushirikiano huu kwa kutoa taarifa kuhusu viwango na tathmini; kutoa mafunzo na nyenzo kwa wazazi ili kuwasaidia watoto wao; kuelimisha wahudumu wa shule kuhusu ushirikishaji wa wazazi na thamani ya michango ya wazazi; na kukuza majukumu ya mashirika ya jamii na biashara ili kushirikiana na wazazi na shule.

1. Sera hii ya maandishi iliyoundwa na kukubaliwa kwa pamoja itasambazwa kwa wazazi na wanafamilia wa watoto wa Title I wanaoshiriki kielektroniki mwanzoni mwa mwaka wa shule. Katika majengo ya schoolwide, hii itajumuisha wazazi wote. (ESSA Sehemu ya 1116(a)(2))

2. Wilaya itatoa usaidizi wa kiufundi na msaada kwa shule kwa kupanga na kutekeleza shughuli za kufana za ushirikishaji wa wazazi na familia ili kuboresha ufanisi wa elimu ya wanafunzi na utendaji wa shule kupitia maendeleo ya kitaalamu kuhusu ushirikishaji wa wazazi na familia. Wilaya itashirikiana na makundi ya jamii kama njia ya kuzishirikisha familia kwa ubunifu na ufanisi zaidi. (ESSA Sehemu ya 1116(a)(2)(B))

3. Wilaya itajitahidi kupata njia za kushirikiana na mipango mingine ya Serikali kuu, jimbo na serikali ya mtaa. Mpango wa Title I utashirikiana na afisa wa ushirikiano wa wilaya wa ukosefu wa makao, mpango wa elimu ya mapema na mipango ya elimu maalum (IDEA). (ESSA Sehemu ya 1116(a)(2)(C))

4. Wilaya itafanya tathmini ya kila mwaka ya maudhui na ufanisi wa Sera ya Ushirikishaji wa Wazazi na Familia. Zana na mbinu za tathmini zinatambua aina na mara za miingiliano ya shuleni na nyumbani na mahitaji ya wazazi na famili ili kuwasaidia vyema watoto wao kusoma. Tathmini zitalenga angalau sehemu tatu muhimu: Vizingiti, uwezo wa kusaidia kusoma na miingiliano yenye ufanisi. (ESSA Sehemu ya 1116(a)(2)(D)(i-iii))

5. Wilaya itatumia matokeo ya tathmini ya kila mwaka kuunda mikakati kulingana na ushahidi kwa ajili ya ushirikishaji wa wazazi na familia wa kufana zaidi. Matokeo ya tathmini yatasaidia kubainisha desturi bora zinazofaulu na kutumia hoja hizo kwenye mahitaji ya wilaya na shule husika. (ESSA Sehemu ya 1116(a)(2)(E))

6. Wilaya inashirikisha wazazi na wanafamilia katika shughuli za shule kupitia mawasiliano na miingiliano ya mara kwa mara na inaomba mchango wao katika mapitio na marekebisho ya Sera ya Ushirikishaji wa Wazazi na Familia. (ESSA Sehemu ya 1116(a)(2)(F))

7. Angalau mkutano mmoja wa kila mwaka utafanywa ili kuwataarifu wazazi na wanafamilia kuhusu ushiriki wa shule katika mpango wa Title I na kueleza mahitaji ya mpango na haki yao ya kushirikishiwa. Mkutano utakuwa wa wazazi wa shule za umma na za binafsi. Shule zote za elementari zitafanya mkutano wa kila mwaka majira ya majani kupukutika. Arifa itatumwa kwenye jarida la shule. (ESSA Sehemue ya 1116(c)(1))

8. Mikutano ya wazazi na familia, ikiwemo makongamano ya wazazi, itafanywa nyakati tofauti za siku na fedha za Title I zinaweza kutumiwa kulipa gharama zinazofaa na muhimu ambazo zinahusiana na shughuli za ushirikishaji wa wazazi na familia, ikiwemo gharama za usafiri, huduma ya malezi ya watoto, au ziara za nyumbani ili kuwawezesha wazazi kushiriki katika mikutano na vipindi vya mafunzo yanayohusiana na shule. (ESSA Sehemu ya 1116(c)(2))

9. Wilaya itawashirikisha wazazi katika mipango, mapitio na uboreshaji wa mpango wa shule wa Title I kupitia ushiriki katika tafiti na mikutano ya ana kwa ana ambapo wazazi wanatoa mchango na mano. (ESSA Sehemu ya 1116(c)(3))

10. Katika mpango wa schoolwide, wazazi wataombwa kushirikishwa katika uuundaji wa pampja wa mpango wa shule kupitia mikutano ya ana kwa ana, tafiti na maoni ya elektroniki inavyofaa. Hii inahusu tu shule za Title I zinazoendesha Mpango wa Schoolwide. (ESSA Sehemu za 1116(c)(3) na 1114))

11. Wazazi na wanafamilia wa watoto wanaoshiriki watapewa usaidizi wa kuelewa mpango wa Title I, pamoja na taarifa wakati unaofaa kuhusu mpango wa Title I. Kupitia mikutano ya kila mwaka, makongamano ya wazazi na walimu na ripoti za utendaji shuleni, shule itawapa wazazi na wanafamilia wa watoto wanaoshiriki ufafanuzi na maelezo ya mtaala unaotumika shuleni, aina za tathmini ya elimu zinazotumika kupima maendeleo ya mwanafunzi na viwango vya ustadi ambavyo wanafunzi wanatarajiwa kutimiza. Wazazi na wanafamilia wanapokea ufafanuzi wa maelezo ya utendaji wa shule, aina za tathmini za elimu zinazotumika kupima maendeleo ya mwanafunzi na viwango vya ustadi vinavyotarajiwa katika ripoti ya maendeleo ya kila mwaka inayowasilishwa majira ya majani kupukutika ya mwaka, kupitia ripoti za binafsi zinazopewa wazazi wakati wa kongamano na kupitia ripoti za utendaji wa mwanafunzi. (ESSA Sehemu ya 1116(c)(4)(A) & (B))

12. Shule ikiombwa na wazazi, itatoa nafasi ya mikutano ya mara kwa mara ili kutoa mapendekezo na kushiriki, inavyofaa katika maamuzi yanayohusiana na elimu ya watoto wao na kujibu mapendekezo yoyote kama hayo haraka iwezekanavyo. (ESSA Sehemu ya 1116(c)(4)(C))

13. Ikiwa mpango wa schoolwide chini ya Sehemu ya 1114(b) hauridhishi, wazazi wa wanafunzi wanaoshiriki wanaweza kutoa maoni. Maoni yanaweza kupewa mwalimu mkuu wa shule kwa njia ya maandishi. (ESSA Sehemu ya 1116(c)(5))

14. Mkataba wa shule/wazazi ulioundwa pamoja unaainisha jinsi wazazi na wanafamilia, wafanyakazi wote wa shule na wanafunzi wanavyoshiriki jukumu la ufanisi wa wanafunzi ulioimarika. Mkataba pia unaelezea njia ambazo shule na wazazi watatumia kujenga na kukuza ushirikiano ili kuwasaidia wanafunzi kufanikisha viwango vyetu vya juu vya ndani. Utasambazwa wakati wa usajili na kupitiwa kwenye mikutano ya kila mwaka. (ESSA Sehemu ya 1116(d))

15. Wazazi wataarifiwa kuhusu sera hii kwa muundo unaoeleweka na mmoja na kwa kiwango

kinachowezekana, kutolewa kwa lugha ambayo wazazi wanaweza kuelewa. Sera itatolewa kwa Kiingereza, kutafsiriwa kwa lugha nyinginezo na haitakuwa na misamiati ya kielimu. (ESSA Sehemu ya 1116(b)(1))

16. Ili kuhakikisha ushirikishaji faafu wa wazazi na kusaidia ushirikiano miongoni mwa shule, wazazi na jamii zinazolenga kuimarisha mafanikio ya elimu ya wanafunzi, kila shule na shirika la elimu la karibu:

    a. Zitatoa usaidizi kwa wazazi kuelewa viwango vya elimu vya jimbo vyenye changamoto, tathmini za elimu za jimbo na serikali ya mtaa, jinsi ya kufuatilia maendeleo ya watoto na kushirikiana na walimu ili kuimarisha mafanikio ya watoto wao;

    b. Zitatoa nyenzo na mafunzo ili kuwasaidia wazazi kushirikiana na watoto wao kuimarisha mafanikio ya watoto wao, kama vile mafunzo ya elimu na kutumia teknolojia (ikiwemo elimu kuhusu madhara ya wizi wa hakimiliki), inavyofaa, ili kuendeleza ushirikishaji wa wazazi;

    c. Zitawaelimisha walimu, wafanyakazi wasaidizi wa mafunzo maalum, walimu wakuu na viongozi na wafanyakazi wengine wa shule, kwa usaidizi wa wazazi, katika thamani na matumizi ya michango ya wazazi na jinsi ya kuwasiliana na kushirikiana na wazazi kama washirika sawa, kutekeleza na kuratibu mipango ya wazazi na kujenga uhusiano baina ya wazazi na shule;

    d. Zitaratibu na kujumuisha mipango na shughuli za ushirikishaji wa wazazi pamoja na mipango ya Serikali Kuu, Jimbo na serikali ya mtaa, ikiwemo mipango ya umma ya shule ya chekechea na kufanya shughuli nyingine kama vile vituo vya huduma kwa wazazi, zinazowahimiza na kuwasaidia wazazi kushiriki kikamilifu zaidi katika elimu ya watoto wao;

    e. Zitahakikisha kuwa taarifa zinazohusiana na mipango ya shule na wazazi, mikutano na shughuli nyingine zinatumwa kwa wazazi wa watoto wanaoshiriki kwa muundo na kwa kiwango kinachowezekana kwa lugha ambayo wazazi wanaweza kuelewa; na

    f. Zitatoa msaada mwingine kama huo unaofaa kwa shughuli za ushirikishaji wa wazazi chini ya sehemu hii kama wazazi wanavyoweza kuomba. (ESSA Sehemu ya 1116(e)(1-14))

17. Shule itatoa nafasi kwa kiwango kinachowezekana kwa ushiriki ambao wazazi na wanafamilia wanafahamu (ikiwemo wazazi na wanafamilia walio na ustadi kidogo wa Kiingereza, wazazi na wanafamilia walio na ulemavu na wazazi na wanafamilia wa watoto wahamiaji) kwa kutoa taarifa na ripoti za shule zinazohitajika chini ya Sehemu ya 1111 kwa muundo na lugha ambayo wahusika wanaweza kuelewa.

# Title I Mkataba wa Wazazi

**Iowa City Community School District**
1725 North Dodge Street • Iowa City, IA 52245 • (319) 688-1000 • Faksi (319) 688-1009
www.iowacityschools.org

Wanafunzi wanaosomea Alexander, Borlaug, Central, Hills, Hoover, Horn, Kirkwood, Longfellow, Lucas, Twain, Weber na Wood wanastahiki kupokea huduma kutoka kwenye mpango wa Title I. Title I imeundwa ili kutoa msaada wa mafunzo katika kusoma (na ikiwezekana hisabati) na walimu waliohitimu zaidi siku ya shule. Tafadhali pitia mkataba huu na uwasiliane na shule ya mtoto wako ukiwa na swali lolote.

## Malengo kwa wanafunzi walio katika mipango:

Malengo ya Kusoma yanaweza kujumuisha:

- Kuongeza ufahamu wa fonimu na stadi za fonetiki
- Kuongeza utambuzi wa maneno ya kuona katika kusoma na kuandika
- Kuongeza ufasaha wakati wa kusoma na kuandika maandishi/maneno yanayofahamika
- Kuongeza matumizi ya mikakati mingi wakati wa kusoma na kuandika maandishi/maneno yasiyofahamika
- Kuongeza ufahamu na uwezo wa kusimulia hadithi kwa mdomo na kwa maandishi

Malengo ya Hisabati yanaweza kujumuisha:

- Kuongeza uelewa wa sehemu ya namba kamili
- Kuongeza ustadi wa ujumlishaji, utoaji, uzidishaji na ugawaji msingi
- Kuongeza matumizi ya mikakati inayofaa kutatua matatizo
- Kuongeza uwezo wa kuonyesha fikira za kihisabati kwa marika, walimu na wengine

## Je, mafunzo haya yanatolewa vipi katika Mpango wa Title I?

Wanafunzi wanashiriki katika mafunzo ya ana kwa ana au kikundi kidogo na mwalimu wa Title 1 au mwalimu wa darasa. Walimu wa Title 1 na walimu wa darasa wanashirikiana kuratibu mafunzo ya elimu au hisabati yanayotolewa katika mazingira ya darasa na ya kikundi.

## Je, kwa nini ushirikishaji wa wazazi ni muhimu?

Kulingana na utafiti, ushirikishaji wa wazazi ni jambo muhimu kwa mafanikio ya elimu ya watoto. Kwa hivyo, ushirikishaji wa wazazi una jukumu muhimu kwa uundaji wa miongozo kwa ajili ya mipango ya kusoma. Walimu hupanga mikutano ili:

- Kushiriki hoja za kusoma na kuandika na mikakati inayoweza kusaidia nyumbani
- Kuwapa wazazi nyenzo za kutumia nyumbani
- Kujibu maswali ambayo wazazi wanayo kuhusu mipango ya kusoma au hisabati

## Jukumu la Mzazi/Mlezi

Ninataka mtoto wako afanikiwe. Kwa hivyo, nitamhimiza kwa kufanya yafuatayo:

- Kuhakikisha kuwa mtoto wangu anaenda shuleni mara kwa mara na bila kuchelewa.
- Kuanzisha tabia ya kusoma na mtoto wangu kila siku kwa dakika 10-30
- Kumfanya mtoto wangu kuniona nikisoma na kuandika (kuwa mfano bora).
- Kushiriki katika makongamano na shughuli.
- Kusoma majarida na kujadili shughuli na mtoto wangu.

Jina la Mtoto: ________________________________________ Shule: __________________________

Sahihi ya Mzazi: ______________________________________ Tarehe: ____________________________

*Updated October 2021*

Dhamira ya Iowa City Community School District ni kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wanawajibika, kuwa wanafunzi wa kujitegemea wanaoweza kufanya maamuzi ya busara katika jamii yenye demokrasia na pia katika jamii ya kimataifa inayobadilika; hili linafanikishwa kwa kumpa changamoto kila mwanafunzi na mtaala wa kina na wenye ubunifu unaofunzwa na wafanyakazi wenye utofauti, wataalam na wanaojali na walioimarishwa kupitia rasilimali na jitihada za familia na jamii nzima.

*Updated October 2021*